**Noa Bongo !Jenga Maisha Yako!**

**Utandawazi :Kujumuika kwa Mafanikio katika Jamii Ujerumani**

**Reportage : Konstanze von Kotze**
**Redaktion : Sandrine Blanchard**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen : Sauti 3**

- **junger Sprecher 1 …………….Msimulizi wa kiume 1**
- **junge Sprecherin 1 …………..Msimulizi wa kike 1**
- **Sprecher(in) 2 ……………….Msimulizi wa kike 2**
  **als Off-Stimme für die Reportage**

  **Für die O-Ton dazu :**
  **I junge Frau - Sauti ya kike 1**

---

**Vorspann LbE…………………………..Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA - REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :**

Habari gani ! Natumai nyote hamjambo !

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Leo katika mfululizuo wetu wa Noa Bongo!Jenga Maisha Yako! kuhusu utandawazi tutakutana na Edith.

**Msimulizi wa kike 1 :**

Mwanamke wa Cameroon ambaye amekuwa akiishi nchini Ujerumani kwa miaka mingi na kuweza kujipatia ajira pamoja na kufanikiwa kujumuika kwenye jamii.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Na tutakuwa tunaelekea kwenye mji wa Bonn ambako ndiko anakoishi Edith.

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari !

**……………………Manuscript……………………**

1. **Atmo hoch unterlegen**
   **mere + fils rangent le cartable qui pese trop lourd …………**

   **Msimulizi wa kike 2 :**

   Edith ana umri wa miaka 27.Ni mwananchi wa Cameroon mwenye kuzungumza lugha ya Kingereza.Mtoto wake wa kiume pia amezaliwa Cameroon lakini amekulia nchini Ujerumani.Yeye anazungumza na kufahamu Kingereza ambayo kwake ni lugha mama kadhalika Kijerumani lugha aliyokulia nayo ……

   **2 Atmo : Mother/son ….exchange in German and English ………Mama/ mtoto wakiongea Kijerumani na Kingereza…….**

   **Msimulizi wa kike 2 :**

   Mama na mtoto wake huyo wa kiume wamekuwa wakiishi Ujerumani ya magharibi kwa takriban miaka minane sasa. Edith amekuja nchini Ujerumani wakati alipokuwa ana umri wa miaka 19 kujiunga na mama yake aliyekuweko Bonn. Hapo ndipo kazi pevu ya kutafuta kazi ilipoanza.

   **2.O-Ton Edith**

   Niliwahi kufanya kazi kwenye mkahawa,kwenye McDolands na katika hospitali.Baadae nikaanza kwenda madarasani juu ya kwamba haikuwa rahisi kujiandikisha kwenye

mafunzo.Ilinichukuwa miaka miwili kujiunga na baadae ilikuwa nikihitaji miaka mitatu kukamilisha mafunzo kwa sababu yalikuwa kwa lugha ya Kijerumani.Na kwa vile nilikuwa nimehudhuria shule wakati nilipokuwa Cameroon ilinibidi nivitafsirishe vyeti vyangu vyote ili kwamba waweze kuvitambuwa.Haikuwa rahisi.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Kwa hiyo kimsingi Edith alikuwa akifanya kazi duni kwa miaka minane ?

**Msimulizi wa kike 1 :**

Hapana….aliweza kupata kazi ya maana katika Deutsche Post …shirika la posta la Ujerumani.

**3.O-Ton Edith**

Nilikuwa nikishindana na Wajerumani, watoto waliokulia hapa ambao wanaijuwa lugha yao vizuri zaidi kuliko mimi. Lakini nilikuwa na bahati ……kwamba kazi zote ninazopata ilikuwa ni kwa sababu walikuwa wakihitaji mtu anayezungumza Kingereza.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Edith anaishi na mtoto wake wa kiume katika nyumba nzuri. Ilibidi ajinyime kuweza kufikia hatua hii na kuvumilia kusemwa na hata matusi.Watu walikuwa hawakumpa uzito
kwa sababu alikuwa mwanamke ,alikuwa mweusi na alikuwa kijana …..lakini alikuwa hajali.

**4.O-Ton Edith**

Nilikuwa sijali …..niliwapuuza kwa sababu siku zote kulikuwa na watu wakiniangalia kwa mshangao.Ilikuwa ikinibidi kuwathibitishia kwamba nilikuwa nastahili kazi hii na nilikuwa tayari kufanya kitu chote chote kile kupigania kufanikisha maisha yangu.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Wakati alipowasili Ujerumani Edith hakuwa amefikri kwamba ingelikuwa vigumu sana kujiambatanisha na jamii. Aliuona mji wa Bonn kuwa ni mzuri lakini pia alidhani kuwa Wajerumani ni watu waliosongwa na mambo.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

Kwa kweli Ulaya sio kama vile watu wanavyoielezea huko barani Afrika.

**5. O-Ton Edith**

Habari wanazozipata watu wakiwa huko zinasema kwamba Ulaya ni nzuri zaidi ……daima huwa wanafikiria kwamba maisha mazuri yako Ulaya.Lakini sifikiri hivyo.Kama inavyosemwa ikiwa huwezi kuzungumza lugha husika huwezi kujuwa.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Kuna picha za familia yake na marafiki zake kwenye kuta za chumba chake cha kupumzikia.Edith anaendelea kuwa na mawasiliano na famili yake ilioko Cameroon licha ya kwamba yuko mbali sana na nyumbani.

**6.O-Ton Edith**

Siku zote huwa nawapigia simu.Tunatumiana baruwa pepe lakini huwa tunazungumza kwa simu kila ya baada ya siku moja.Naitamani familia yangu na najuwa wao pia wananitamani.Lakini hayo ndio maisha.Mara nyengine maisha yanakuwa ya ajabu …..daima huwa tunataka kwenda nyumbani kwa sababu huko huwa tuanajisikia kufarajika zaidi…. lakini tunayakubali maajaliwa yetu…….

**Msimulizi wa 2 :**

Edith anataraji iko siku atarudi tena Cameroon.Lakini kwa hivi sasa anajaribu kumfundisha mtoto wake wa kiume juu ya tamaduni zote mbili ……kuhusu lugha,muziki,chakula……

**Atmo Aufzählung Gerichte ……………………..**

**7.O-Ton Edith**

Ni muhimu kwake kujuwa anatoka wapi, tunakula chakula gani huko nyumbani …..ili iwapo ikibidi arudi nyumbani mambo yasio mageni kwake.

**Msimulizi wa kike 2 :**

Lakini Edith anafahamu kwamba ni muhimu kwa mtoto wake huyo kujumuiaka vizuri katika jamii nchini Ujerumani.Bonn ni dunia nyengine lakini pia ni dunia ya mtoto wake huyo wa kiume.

**8.O-Ton Edith**

Anajisikia vizuri hapa juu ya kwamba mara nyengine anakuwa na matatizo shuleni wakati wenzake wanapomuita Muafrika. Watoto ambao wameelimishwa vibaya humtendea mwanangu vmambo yasio mazuri  huko shule lakini yuko imara. Huwa wanamtukana……… wanampachika majina machafu lakini anajuwa namna ya kujihami.

**Atmo toothbrushing ………kupiga mswaki……**

**Msimulizi wa kike 2 :**
Edith anasema atamuunga mkono mwanawe iwapo iko siku atataka kurudi Cameroon.

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

**Jingle Noa Bongo!Jenga Maisha Yako !**

---

**SEHEMU YA PILI : ERKLÄRSTÜCK**

**Msimulizi wa kiume :**

Mwanzoni Edith alizungumzia juu ya vyeti vyake vya Cameroon kwa kutotambuliwa mara moja wakati alipowasili nchini Ujerumani.

**Msimulizi wa kike :**
Iwapo watu hawatokei katika nchi za Umoja wa Ulaya ili kujiandikisha katika Chuo Kikuu cha Ujerumani inabidi wathibitishe kwamba wana sifa zinazostahiki.

**Msimulizi wa kiume :**
Kwa hiyo inabidi wathibitishe kwamba wana vyeti vya kumalizia shule ili kuweza kushiriki kwenye madarasa katika Chuo Kikuu?

**Msimulizi wa kike :**
Hivyo ndivyo ilivyo kimsingi.Lakini unaweza ukafikiria kwamba maafisa wa Ujerumani hawawezi kusoma vyeti vyote katika lugha zote.Kwa hiyo mtu mwenye kutafsiri vyeti anatakiwa atafsiri vyeti hivyo katika lugha inayotambuliwa rasmi.

**Msimulizi wa kiume :**
Kuna matatizo machache barani Afrika kuhusiana na kutambuliwa kwa vyeti na stashahada.

**Msimulizi wa kike :**
Hiyo ni kwa sababau ya Makubaliano ya Umoja wa Mataifa ambayo yalitiwa saini na takriban nchi zote katika bara hilo mapema miaka ya 1980.

**Msimulizi wa kiume :**
Kitu kama hicho kinahitajika kati ya Ulaya na Afrika !

Msimulizi wa kike :
Huenda iko siku kukawepo na kitu hicho.Lakini sio hayo tu ili uweze kujifunza nchini Ujerumani inabidi pia uthibitishe kwamba una ujuzi wa kutosha wa lugha kuweza kufahamu masomo.

**Msimulizi wa kiume (proudly …..kwa ufahari ) :**
Ich liiiiebe dich……Hiyo inamaanisha Nakupenda kwa Kijerumani.

**Msimulizi wa kike :**
Ndio lakini hayo ni maneno pekee unayoyajuwa huenda yasitoshe kuweza kufahamu kile anachosema mhadhiri!

**Msimulizi wa kiume :**
Najuwa kusema hujambo yaani… guten Tag (Msimulizi wa kike anacheka )……sawa enhhh.Kwa hiyo unafanya nini wakati unapokuwa huwezi kusema Kijerumani?

**Msimulizi wa kike :**
Inabidi uwende kwenye masomo ya lugha.Kwa njia hiyo unaweza kupata cheti cha lugha kabla ya muhula wa masomo ya Chuo Kikuu kuanza.Kuna aina mbali mbali …kwa mfano kama testDAF au DSH.Vinathibitisha kwamba una ujuzi wa kiwango cha lugha sawa na kile cha mwanafunzi wa sekondari wa Kijerumani.Pia inasaidia iwapo umechukuwa masomo ya Kijerumani katika nchi ulikozaliwa.

**Msimulizi wa kiume :**
Wapi naweza kujifunza Kijerumani barani Afrika?
Msimulizi wa kike :
Kuna taasisi ya Goethe katika nchi 16 za Afrika.Pia kuna vituo vya utamaduni vya Kijerumani ambavyo pia vinaendesha masomo ya lugha.Venginevyo kuna masomo ya Kijerumani katika mtandao na siku zote kunakuwepo na vitabu vya kujifunzia.

**Msimulizi wa kiume:**
Alaaa. Na inakuwaje iwapo unashindwa mtihani wa lugha ?

**Msimulizi wa kike :**
Makamo Chansellor atakumeza ukiwa hai!

**Msimulizi wa kiume (effreye) :**
Nini ? Lazima utakuwa unatania !

**Msimulizi wa kike :**
Ndio natania! Ikiwa utashindwa mtihani inabidi utumie miezi kadhaa katika Studienkolleg (Chuo cha Mafunzo )ili kuweza kufikia kiwango kinachotakiwa na kufanya tena mtihani huo. Mara unapopata cheti chako unaweza kujiandikisha katika madarasa ya chuo kikuu.

**Outro ……………………..Funga kipindi…………..**

Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Noa Bongo! Jenga Maisha Yako!Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na kujumuika katika jamii nchini Ujerumani. Ni kipindi kilichotayarishwa na Konstanze von Kotze na Sandrine Blanchard.Ili kujuwa zaidi na iwapo ungelipenda kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu :
www.de-worl.de/be.
Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine!
Kwaheri.